



## Uundaji wa Kauli ya Kutendwa Katika Lugha ya Kiswahili na ya Kiarabu

Ibrahim Elhadi Mohamed Lehmedi

Idara Ya Lugha Na Taaluma Za Kiafrika, Kitivu Cha Sanaa, Chuo Kikuu Cha Sebha, Libya

### Keywords:

Irabu  
Kauli ya kutendwa  
Kiambishi mnyambuliko  
Mtenda  
Mtendwa  
Uundaji

### ABSTRACT

Utafiti huu unalenga kuchanganua na kuchunguza uundaji wa kauli ya kutendwa katika lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu, na mtafiti kutokana na ufundishaji wake wa kozi za sarufi kwa wanafunzi wanaojifunza lugha Kiswahili katika Idara ya lugha na Taaluma za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Sebha kwa muda mrefu, mtafiti aliona kuwa kuna wanafunzi wengi wanakumbana na matatizo mengi na ugumu wa kuelewa jinsi na kanuni za uundaji wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa mtafiti anaelekea kwenye dhana kwamba tofauti kati ya lugha hizo mbili katika jinsi na kanuni za uundaji wa kauli ya kutendwa ni sababu mojawapo ya kuwepo kwa baadhi ya matatizo na ugumu. Kwa hivyo, mtafiti alichunguza jinsi ya kubadilisha vitenzi kuwa katika kauli ya kutendwa kisha kuvitumia katika sentensi ili mwanafunzi ajue jinsi na kanuni za uundaji wa kauli ya kutendwa katika lugha zote mbili Kiswahili na Kiarabu. Ifahamike hapa kuwa utafiti huu unachukuliwa kuwa wa kwanza wa aina yake kwa kuwa ulishughulikia maelezo ya jinsi ya kuunda kauli ya kutendwa katika lugha ya Kiarabu kwa lugha ya Kiswahili, pamoja na kwamba unachanganya katika kueleza uundaji wa kauli ya kutendwa katika Kiswahili na Kiarabu katika utafiti huo huo. Mwenyezi Mungu akipenda, utafiti huu utakuwa wa thamani si tu kwa wanafunzi wa Kiarabu wanaojifunza lugha ya Kiswahili, bali pia kwa wanafunzi wa Kiswahili wanaojifunza Kiarabu. Pia, utafiti huu utawasaidia katika kujua jinsi ya kuunda kauli ya kutendwa katika lugha ya Kiarabu na tofauti na lugha ya Kiswahili. Isitoshe, bali faida itakuwa hata kwa walimu na watafiti wa lugha zote mbili.

## بناء المبني للمجهول في اللغة السواحيلية واللغة العربية

ابراهيم الهادي محمد لحميدي

اللغات الإفريقية، كلية الآداب، جامعة سبها، ليبيا

### الكلمات المفتاحية:

المبني للمجهول  
بناء  
حركة  
فاعل  
لاحقة الاشتقاق  
مفعول به

### الملخص

يهدف هذا البحث الى تحليل ودراسة بناء المبني للمجهول في اللغة السواحيلية واللغة العربية وقد لاحظ الباحث من خلال تدريسه مادة الصرف لطلاب اللغة السواحيلية بقسم اللغات الإفريقية بجامعة سبها لفترة طويلة لاحظ ان كثيرا من الطلاب يواجهون بعض المشاكل والصعوبات في فهم كيفية بناء الأفعال في اللغة السواحيلية. حيث ان الباحث يميل الى فرضية أن الاختلاف بين اللغتين في كيفية صياغة المبني للمجهول هي احد الأسباب في وجود بعض هذه المشاكل والصعوبات. عليه فقد قام الباحث بدراسة كيفية تحويل الأفعال الى المبني للمجهول، ومن بعد ذلك استخدامها في جمل حتى يتسنى للطلاب معرفة الكيفية والقوانين التي تم بها صياغة المبني للمجهول في كلتا اللغتين السواحيلية والعربية. وتصدر الإشارة هنا الى ان هذا البحث يعد البحث الأول من نوعه من حيث أنه يتناول شرح كيفية بناء المبني للمجهول في اللغة العربية باللغة السواحيلية بالاضافة الى أنه يجمع في شرحه بناء المبني للمجهول في اللغة السواحيلية والعربية في البحث نفسه. سيكون هذا البحث ان شاء الله ذا قيمة ليس فقط للطلاب العرب الدارسين للغة السواحيلية بل وحتى الطلاب السواحيليين الذين يتعلمون اللغة العربية. وكذلك

\*Corresponding author:

E-mail addresses: [ibr.lehmedi@sebhau.edu.ly](mailto:ibr.lehmedi@sebhau.edu.ly)

Article History : Received 28 February 2022 - Received in revised form 20 August 2022 - Accepted 20 September 2022

فان هذا البحث يساعد في معرفة كيفية بناء المبني للمجهول في اللغة العربية، وأوجه الاختلاف مع اللغة السواحيلية. وليس هذا فحسب بل ان الفائدة ستكون حتى للمدرسين والباحث في كلتا اللغتين.

## UTANGULIZI

Kwa kawaida Kitenzi kimoja kinaweza kudhihirisha hali tofauti za vitendo. Kuna hali kama vile hali ya kauli ya kutenda, kauli ya kutendea, kauli ya kutendana, kauli ya kutendwa, kauli ya kutendeka na kauli ya kutendesha na katika lugha mbalimbali duniani.

Kwa mujibu wa Baraka (2018), mnyambuliko wa vitenzi ni jambo muhimu sana katika lugha zote. Kulingana na maelezo yake, mnyambuliko wa vitenzi hupelekea kitenzi kimoja kuleta maana tofauti tofauti kutokana na hali mbalimbali za mnyambuliko

Kihore, Y ( 2012 ) Mengi ya maandishi yanaonyesha kuwa kuna wasomi wengi sana ambao wameandika kuhusu mnyambuliko wa vitenzi katika lugha zote duniani. Kuna wasomi ambao wameandika kuhusu mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili na kuna wale ambao wameandika kuhusu mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kiarabu kwa lugha ya Kiarabu. Hata hivyo, hakuna ushahidi kuwa kuna mtaalamu yeyote ambaye ameanadika kuhusu mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kiarabu ameanadika kwa lugha ya Kiswahili.

## SUALA LA UTAFITI

Kwa mujibu wa mtafiti, na kutokana na uzweifu wake wa kufundisha Kiswahili na hasa kozi za kisarufi kwa wanafunzi wa Kiarabu nchini Libya kwa zaidi ya miaka kumi na nane hadi sasa hivi, mtafiti aliona kwamba kuna wanafunzi wengi sana wa Kiarabu wanaojifunza Kiswahili wanakumbana na matatizo mbalimbali ya kisarufi na hasa upande wa mnyambuliko wa vitenzi (kauli za vitenzi).

Wengi wa walimu na wanafunzi wana shida ya kuelewa jinsi na kanuni za kuunda kauli za vitenzi katika lugha zote mbili Kiswahili na Kiarabu. Kutokana na matatizo hayo, na ili krahisha mamabo hayo mtafiti aliamua kuendeleza utafiti huu akidhamiria kuelewa jinsi ya kuunda kauli ya kutendwa tu katika lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu kwa lugha ya Kiswahili.

## MALENGO YA UTAFITI

Malengo ya utafiti huu ni kuchunguza na kutoa taarifa kuhusu kanunin za kuunda kauli ya kutendwa katika lugha zote mbili Kiswahili na Kiarabu. Ili tuweze kufikia azma hiyo inafaa tuukabili utafiti wetu kwa kuzingatia yafuatayo:

- kutoa taratibu na kanuni za kunyambulisha vitenzi vya lugha Kiswahili na njia za kuunda kauli ya kutendwa pamoja na kutoa mifano katika lugha ya Kiswahili.
- kutoa taratibu na kanuni za kunyambulisha vitenzi vya lugha ya Kiarabu na njia za kuunda kauli ya kutendwa pamoja na kutoa mifano kwa lugha ya Kiarabu kwa lugha ya Kiswahili.
- Kuchunguza sababu za shida ya wanafunzi kuelewa kanuni za mnyambuliko wa vitez vya Kiswahili na hasa kauli ya Kutendwa.

## UMUHIMU WA UTAFITI

Utafiti huu unatarajiwa kuwa na faida kwa wanafunzi wa Kiarabu wanaojifunza Kiswahili, pia utafiti utakuwa na faida kwa wanafunzi wa Kiswahili wanojifunza lugha ya Kiarabu kujua zaidi juu ya kauli ya kutendwa katika lugha ya Kiswahili na ya Kiarabu. Walimu na wataalamu wa Kiswahili watakuwa na fikra kuhusu jinsi ya kuunda kauli ya kutendwa katika lugha ya Kiarabu.

## UUNDAJI WA KAULI YA KUTENDWA KATIKA LUGHA YA KISWAHILI:

Mohamed ( 2006 ) Kauli ya kutenda hueleza jambo ambalo mtendaji ametenda. Kwa kawaida aghalabu ya vitenzi vya

Kiswahili vya kauli ya kutenda huishia na irabu [ -a ] isipokuwa baadhi ya vitenzi vilivyokopwa kutoka lugha za kigeni ambavyo huweza kuishia na irabu [ -e, -i, -o, au -u ].

Khamis ( 2008 ) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili, kama ilivyo na lugha nyingi za Kibantu ina utajiri mkubwa sana wa mfumo wa unyambulishaji wa vitenzi. Idadi kubwa ya shughuli za kisarufi ambazo kwa kawaida huwasilishwa kwa njia ya miundo ya kisintakisia katika lugha zenye uhaba wa msamiati, maneno hudhibitiwa kwa utaratibu wa unyambulishaji wa vitenzi. Katika Kiswahili kwa mfano, unyambulishaji hupelekea kiambishi tamati kiwekwe kwenye umbo la kitenzi

Hali kadhalika, maandishi yaliyosomwa yanaonyesha kuwa si vitenzi vyote katika lugha huwa vinanyambuliwa, kuna vitenzi vinavyonyambuliwa na kuna vile visivyonyambuliwa, Mbwilow, S. N. (2017).

E. Wesana chomi (2001) Kauli ya kutendwa hupatikana wakati tunapofikiria kwamba mtu fulani au kitu fulani kimetendwa. Vitenzi katika kauli hii huchukua viambishi tamati ( viishio ) mbalimbali kama: [ -WA / -IWA / -LEWA / -LIWA ]

### 1. KIAMBISHI [ -WA ]

Kiambishi mnyambuliko [ -WA ] ni mojawapo wa viambishi vinavyotumiwa katika kunyambulisha vitenzi vya Kiswahili vya kauli ya kutendwa. Vitenzi ambavyo vyenye asili ya Kibantu na ambavyo huishia na [Konsonanti + Irabu A] na [ Irabu mbili IA ], tunaongeza kiambishi [ -WA ] badala ya irabu [ A ] ya mwisho. Ama vitenzi vyenye asili ya Kiarabu ambavyo huishia na [ Irabu E ] na [ Irabu I ] tunaongeza kiambishi [ -WA ] mwishoni mwa kitenzi, kama inavyonekana hapa chini:

A. Vitenzi vyenye asili ya Kibantu ambavyo huishia na [ Konsonanti + Irabu A ].

k.m, Kusoma → Kusomwa

Mwanafunzi alisoma kitabu.

Kitabu kilisomwa na mwanafunzi.

B. Vitenzi vyenye asili ya Kibantu ambavyo huishia na [ Irabu mbili IA ].

k.m Kufagia → Kufagiwa

Amina amefagia chumba.

Chumba kimefagiwa na Amina.

C. Vitenzi vyenye asili ya Kiarabu ambavyo huishia na [ Irabu E ].

k.m Kusamehe → Kusamehewa

Mwalimu amesamehe wanafunzi.

Wanafunzi wamesamehewa na mwalimu.

D. Vitenzi vyenye asili ya Kiarabu ambavyo huishia na [ Irabu I ].

k.m Kujadili → Kujadiliwa

Mwalimu amejadili wanafunzi.

Wanafunzi wamejadiliwa na mwalimu.

### 2. KIAMBISHI [ -LIWA ]

Kiambishi mnyambuliko [ -LIWA ] ni mojawapo wa viambishi vinavyotumiwa katika kunyambulisha vitenzi vya Kiswahili vya kauli ya kutendwa. Vitenzi ambavyo vyenye asili ya Kibantu na ambavyo huishia na [ Irabu mbili AA ] na [ Irabu mbili UA ], tunaongeza kiambishi [ -LIWA ] badala ya irabu [ A ] ya mwisho. Ama vitenzi vyenye asili ya Kiarabu ambavyo huishia na [ Irabu mbili AU ], tunaongeza kiambishi [ -LIWA ] mwishoni mwa kitenzi, kama inavyonekana hapa chini:

A. Vitenzi vyenye asili ya Kibantu ambavyo huishia na [ **Irabu mbili AA** ].

k.m Kuvaa → Kuvaliwa

Watoto wanavaa mashati.

Mashati yanawaliwa na watoto.

B. Vitenzi vyenye asili ya Kibantu ambavyo huishia na [ **Irabu mbili UA** ].

k.m Kuchagua → Kuchaguliwa

Hadi anachagua viatu.

Viatu vinachaguliwa na Hadi.

C. Vitenzi vyenye asili ya Kiarabu ambavyo huishia na [ **Irabu mbili AU** ].

k.m Kusahau → Kusahauliwa

Sisi tulisahau Kalamu.

Kalamu zilisahauliwa na sisi.

### 3. KIAMBISHI [ -LEWA ]

Kiambishi mnyambuliko [ -LEWA ] ni mojawapo wa

viambishi vinavyotumiwa katika kunyambulisha vitenzi vya Kiswahili vya kauli ya kutendwa. Vitenzi ambavyo vyenye asili ya Kibantu na ambavyo huishia na [ Irabu mbili EA ] na [ Irabu mbili OA ], tunaongeza kiambishi [ -LEWA ] badala ya irabu [ A ] ya mwisho, kama inavyonekana hapa chini:

A. Vitenzi vyenye asili ya Kibantu ambavyo huishia na [ **Irabu mbili EA** ].

k.m Kupokea → Kupokelewa

Idris alipokea zawadi.

Zawadi zilipokelewa na Idris.

B. Vitenzi vyenye asili ya Kibantu ambavyo huishia na [ **Irabu mbili OA** ].

k.m Kuondoa → Kuondolewa

Askari aliondoa gari.

Gari liliondolewa na askari.

### 4. KIAMBISHI [ -IWA ]

Kiambishi mnyambuliko [ -IWA ] ni mojawapo wa viambishi vinavyotumiwa katika kunyambulisha vitenzi vya Kiswahili vya kauli ya kutendwa. Vitenzi vyenye asili ya Kiarabu ambavyo huishia na [ Irabu U ] tunaongeza kiambishi [ -IWA ] badala ya irabu [ u ] mwishoni mwa kitenzi, kama inavyonekana hapa chini:

A. Vitenzi vyenye asili ya **Kiarabu** ambavyo huishia na [ **Irabu U** ].

k.m Kubusu → Kujaribiwa

Mama amebusu mtoto.

Mtoto amebusiwa na mama.

### 5. SILABI MOJA

Vitenzi vya silabi moja unyambulishaji wake ni tofauti na vitenzi vingine kwa sababu haina kanuni maalum, kama inavyoonekana hapa chini:

A. Vitenzi vya **silabi moja**, kama inavyonekana hapa chini.:

Kula → Kuliwa

Kupa → Kupewa

Wanyama walikunywa maji.

Maji yalinyewewa na wanyama.

### UUNDAJI WA KAULI YA KUTENDWA KATIKA LUGHA YA KIARABU ( المَبْنِي لِلمَجْهُول )

Ahmed Gish (2002), Kitenzi katika lugha ya Kiarabu kimegawanyika katika vigawanyiko kadhaa tofauti, vikiwemo vilivyopita, vilivyopo, na vya sharti, vikiwemo vya elekezi na visivyo elekezi, vikiwemo vitatu na pembe nne na zaidi, kikiwemo kitenzi cha kawaida yaani ( sahihi ) ( الفعل الصحيح ) na vitenzi visivyo vya kawaida yaani vya ( Almoataal ) ( الفعل المعتل ), ambavyo tutavijadili kwa undani katika makala hii.

- **kitenzi cha Kawaida ( Sahihi ) ( الفعل الصحيح )**: Ni kila kitenzi ambacho herufi zake asilia hazina vokali ( حرف علة ), ambacho ni “ *alif, waaw na yaa*”. Kama vile: kukaa (جلس), kuhudhuria (حضر), kuandika (كتب), kusoma (قرأ), kusikia (سمع) n.k
- **kitenzi kisicho cha kawaida ( Almoataal ) ( الفعل المعتل )**: Ni kila kitenzi ambacho herufi yake asilia ilikuwa mojawapo ya vokali (*alif, waw na yaa*) kama vile: kuanguka (وقع), kusema (قال), kubaki (بقي). Kitenzi chenye dosari kimegawanywa katika aina mbalimbali, ni kama ifuatayo:

1- Kitenzi ( Almithal ) ( المثل ) : ambacho herufi yake ya kwanza ilikuwa herufi ya vokali ( حرف علة ). Mfano: kupata (وجد), kuanguka (وقع), panua (وسع).

2- Kitenzi ( Ajwaf ) ( الأجوف ) tupu: ambacho ndicho kilikuwa herufi yake ya pili ilikuwa herufi ya vokali ( حرف علة ). Mfano: alisema ( قال ), alilala ( نام ), aliuza ( باع ).

3- Kitenzi ( Naqis ) ( الناقص ) : ambacho herufi yake ya mwisho ilikuwa herufi ya vokali ( حرف علة ). Mfano: kuita (دعا), kutupa (رمى), kushtaki (شكى).

Kwa mujibu wa Ibrahim Alsamraii (1986) umbo la Kauli ya kutendwa ni muhimu sana kwenye lugha yoyote. Inahusisha kubadilisha umbo na maana ya sentensi kwa kadiri fulani. Katika miundo ya kauli ya kutendwa, mtendwa wa sentensi ya kauli ya kutenda huwa mtenda.

Kwa mfano:

كَتَبَ الطَّالِبُ الدَّرْسَ

Mwanafunzi aliandika somo.

Sentensi hii ni katika kauli ya kutenda na mtenda ni mwanafunzi (الطالب).

كُتِبَ الدَّرْسُ

Somo liliandikwa.



Sentensi hii ni katika kauli ya kutendwa na mtenda mhusika haijulikani)

Sharaf Aldin Alrajhi (1999) Ikumbukwe kila wakati kwamba

tunaweza kuunda miundo ya hali ya kutendwa kutoka vitenzi vielekezi. Katika Kiarabu Vitenzi vya hali ya kutenda na vitenzi vya hali ya kutendwa vinahusiana kwa karib, tofauti kuu kati ya maumbo ni vokali (الحركات) Email Badie (2009).

Kutokana na maelezo ya juu tunaweza kuchunguza jinsi na njia za kuunda kauli ya kutendwa katika lugha ya Kiarabu pamoja na kutoa mifano ili kurahisisha maelezo.

**1- VITENZI VYA KIMSINGI VYA KAWAIDA ( Sahihi ) ( الفعل الصحيح )**

Ili kuunda kauli ya kutendwa, tunabadilisha vokali (الحركات) kwenye

TAFSIRI	UNUKUZI	Kitenzi katika kauli ya kutendwa	TAFSIRI	UNUKUZI	Kitenzi katika kauli ya kutenda
-naandikwa	yuktabu	يُكْتَبُ	-naandika	yaktubu	يَكْتُبُ
-naliwa	yu'kalu	يُؤْكَلُ	-nakula	ya'kulu	يَأْكُلُ
-nanywewa	yuShrabu	يُشْرَبُ	-nakunywa	yashrabu	يَشْرَبُ
-nashitakiwa	yuhakamu	يُحَاكَمُ	-nashitaki	yuhākimu	يُحَاكِمُ
-nashereheka	yuhta falu	يُحْتَفَلُ (بـ)	-nashereheka	yahtafilu	(يَحْتَفِلُ بـ)
-nakubaliwa	yutaqabbalu	يُنْقَلَبُ	-nakubali	yataqabbalu	يَنْقَلِبُ
-natolewa	yustakhraju	يُسْتَخْرَجُ	-natoa	yastakhriju	يَسْتَخْرِجُ
-napokelewa	yustaqbalu	يُسْتَقْبَلُ	-napokea	yastaqbilu	يَسْتَقْبِلُ

tuangalie mifano ifuatayo na tutambue mabadiliko kwenye sentensi:

Kauli ya kutendwa (uliopo)	المبني للمجهول ( المضارع )	Kauli ya kutenda (uliopo)	المبني للمعلوم ( المضارع )
Bidhaa zinabebwa kutoka Malaysia.	تُحْمَلُ البَضَائِعُ مِنَ ماليزيا.	Treni inabeba bidhaa kutoka Malaysia.	يَحْمِلُ القطارُ البَضَائِعَ مِنَ ماليزيا.
Somo linaelezwa.	يُشْرَحُ الدَّرْسُ.	Mwalimu anaeleza som.	يُشْرَحُ الأستاذُ الدَّرْسَ.
Mapapai yanapandwa nchini Tanzania.	يُنزَعُ البَابِي فِي تانزانيا.	Watu wanapanda mapapai nchini Tanzania.	يُنزَعُ القاسمُ البَابِي فِي تانزانيا.
Ramadhani inafungwa.	يُصَامُ رَمَضَانَ.	Waislamu wanafunga Ramadhani.	يُصُومُ المسلمونَ رَمَضَانَ.
Quran Tukufu inahifadhiwa.	يُحْفَظُ القُرْآنُ الكَرِيمُ.	Wanafunzi wa Kiislamu wanahifadhi Qur'ani Tukufu.	يُحْفَظُ الطُّلَّابُ المُسْلِمُونَ القُرْآنَ الكَرِيمَ.

**• Namna ya kuunda kauli ya kutendwa katika wakati uliopita**

Ili kubadilisha kitenzi cha wakati uliopita kutoka kauli ya kutenda hadi kauli ya kutendwa, inabidi tufanye mambo mawili kama ifuatavyo:

1-Badilisha vokali (الحركات) ya herufi ya kwanza kuwa dhammah.

TAFSIRI	UNUKUZI	kitenzi kwenye kauli ya kutendwa	TAFSIRI	UNUKUZI	kitenzi kwenye kauli ya kutenda
-liandikwa	Kutiba	كُتِبَ	-liandika	Kataba	كَتَبَ
-liliwa	ukila	أُكِلَ	-likula	Akala	أَكَلَ
-linyewewa	Shuriba	شُرِبَ	-likunywa	Shariba	شَرِبَ
-liingizwa	udkhila	أُدْخِلَ	-liingiza	Adkhala	أَدْخَلَ
-lishitakiwa	hūkima	حُوكِمَ	-lishitaki	Hākama	حَاكَمَ
-lishereheka	uhtufila	أُحْتَفِلَ بـ	-lishereheka	Ihta fala	إِحْتَفَلَ بـ
-likubaliwa	tuqabbila	تُنْقَلَبُ	-likubali	taqabbala	تَنْقَلِبُ
-litolawa	istukhrija	أُسْتَخْرَجَ	-litoa	istakhraja	إِسْتَخْرَجَ
-lipokelewa	ustuqbilla	أُسْتَقْبِلَ	-lipokea	istaqbala	إِسْتَقْبَلَ

nyakati kama ilivyotajwa hapa chini:

- **Namna ya kuunda kauli ya kutendwa katika wakati uliopo**

Katika sehemu hii tutachunguza jinsi ya kubadilisha kitenzi cha wakati uliopo cha Kiarabu kutoka kauli ya kutenda hadi kauli ya kutendwa. Ili kubadilisha kitenzi cha wakati uliopo kutoka kauli ya kutenda hadi kauli ya kutendwa, inabidi tufanye mambo mawili kama ifuatavyo:

1-Badilisha vokali (الحركات) ya herufi ya kwanza kuwa dhammah.

2-Badilisha vokali (الحركات) ya herufi ya kabla ya mwisho kuwa fathah.

tuangalie mifano ifuatayo na tutambue mabadiliko yaliyotokea kwa herufi ya kwanza na herufi ya kabla ya mwisho pamoja na pahali pa vokali.

2-Badilisha vokali (الحركات) ya herufi ya kabla ya mwisho kuwa

TAFSIRI	UNUKUZI	Kitenzi katika kauli ya kutenda
-liandika	Kataba	كَتَبَ
-likula	Akala	أَكَلَ
-likunywa	Shariba	شَرِبَ
-lishitaki	Hākama	حَاكَمَ
-lishereheka	Ihta fala	إِحْتَفَلَ بـ
-likubali	taqabbala	تَنْقَلِبُ
-litoa	istakhraja	إِسْتَخْرَجَ
-lipokea	istaqbala	إِسْتَقْبَلَ

tuangalie mifano ifuatayo na tutambue mabadiliko kwenye sentensi:

المَبْنِي لِلْمَعْلُومِ (الماضي)	المَبْنِي لِلْمَجْهُولِ (الماضي)	Kauli ya kutenda (uliopita)	Kauli ya kutendwa (uliopita)
فَرَشَتِ الْأَمْرَةَ الْبَيْتَ الْجَدِيدَ.	فَرَشَ الْبَيْتَ الْجَدِيدَ.	Familia iliandaa nyumba mpya.	Nyumba mpya iliandaliwa.
أَزَالَ مُحَمَّدٌ السَّرِيرَ مِنَ الْغُرْفَةِ.	أَزَالَ السَّرِيرَ مِنَ الْغُرْفَةِ.	Mohammed aliondoa kitanda kutoka chumba.	Kitanda kiliondolewa kutoka chumba.
قَادَ الْقَائِدُ الْجَدِيدُ الْجَيْشَ.	قَبَدَ الْجَيْشَ.	Kiongozi aliongoza jeshi.	Jeshi liliongozwa.
أَسَسَتْ الْحُكُومَةُ جَامِعَةً جَدِيدَةً.	أَسَسَتْ جَامِعَةً جَدِيدَةً.	Serikali ilianzisha chuo kikuu kipya.	Chuo kikuu kipya kilianzishwa.
إِسْتَقْبَلَ الْجُمْهُورُ الْقَرْيُقَ.	أَسْتَقْبَلَ الْقَرْيُقَ.	Mashabiki waliipokea timu.	Timu ilipokelewa.
كَتَبَ الْوَلَدُ الرُّحَاةَ	كَسَبَتِ الرُّحَاةَ	Mvulana alivunja kioo.	Kioo kilivunjwa.
كَتَبَ الطَّالِبُ الدَّرْسَ.	كَتَبَ الدَّرْسَ	Mwanafunzi aliandika somo.	Somo liliandikwa.

Hebu tuangalie muhtasari wa vitenzi vya kawaida ya kauli ya kutenda na kutendwa katika wakati uliopo na uliopita:

المَبْنِي لِلْمَعْلُومِ (المضارع)	المَبْنِي لِلْمَجْهُولِ (المضارع)	المَبْنِي لِلْمَعْلُومِ (الماضي)	المَبْنِي لِلْمَجْهُولِ (الماضي)
يَذْكُرُ	يَذْكُرُ	ذَكَرَ	ذَكَرَ
- nataja	- natajwa	- litaja	- litajwa
يَسْمَعُ	يَسْمَعُ	سَمِعَ	سَمِعَ
- nasikia	- nasikiwa	- lisikia	- lisikiwa
يَأْمُرُ	يَأْمُرُ	أَمَرَ	أَمَرَ
- naamuru	- naamuriwa	- liamuru	- liamuriwa
يَسْأَلُ	يَسْأَلُ	سَأَلَ	سَأَلَ
- nauliza	- naulizwa	- liuliza	- liulizwa
يَقْرَأُ	يَقْرَأُ	قَرَأَ	قَرَأَ
- nasoma	- nasomwa	- lisoma	- lisomwa

**2- VITENZI VISIVYO VYA KAWAIDA: ( Almoताल ) ( الفعل المعتل )**

Vitenzi visivyo vya kawaida katika hali ya kutendwa hufuata uwekaji wa vokali (الحركات) kama ilivyo kwenye vitenzi vya kawaida pamoja na baadhi ya tofauti zimeonyeshwa hapa chini ili kupatana na ruwaza tofauti:

**• NAMNA YA KUUNDA KAULI YA KUTENDWA KATIKA WAKATI ULIOPIA**

- Katika vitenzi vya (Ajjwaf) (اجوف) herufi ya kwanza lazima ipewe *Kasrah*, na herufi ya kabla ya mwisho (yaani alif) lazima ibadilishwe kuwa *yaa* ياء. Kwa mfano:

المَبْنِي لِلْمَعْلُومِ (الماضي)	المَبْنِي لِلْمَجْهُولِ (الماضي)	Kauli ya kutenda (uliopita)	Kauli ya kutendwa (uliopita)
صَامَ	صَمِمَ	- lifunga	- lifungwa
بَاعَ	بَيْعَ	- liuzwa	- liuzwa

Tuagalie mifano kwenye sentensi:

المَبْنِي لِلْمَجْهُولِ (الماضي) Kauli ya kutendwa (uliopita)	المَبْنِي لِلْمَعْلُومِ (الماضي) Kauli ya kutenda (uliopita)
Mwezi wa Ramadhani ilifungwa. شَهْرُ رَمَضَانَ صِيَمَ.	Ali alifunga mwezi wa Ramadhani.. عَلِي صَامَ شَهْرَ رَمَضَانَ.
Kitabu kiliuzwa. الْكِتَابُ بِيْعَ.	Mwenye duka aliuza kitabu. التَّاجِرُ بَاعَ الْكِتَابَ.

- Katika vitenzi vya ( Naqis ) ( ناقص ) vinavyoishia na ( *alif* ), weka *Dhamma* kwenye herufi ya kwanza na weka *Kasrah* kwenye herufi ya kabla ya mwisho, kisha ubadilisha *alif* kuwa *ya* ي.

المَبْنِي لِلْمَجْهُولِ (الماضي) Kauli ya kutendwa (uliopita)	المَبْنِي لِلْمَعْلُومِ (الماضي) Kauli ya kutenda (uliopita)
- <b>lilindwa</b> حُيِّ	- <b>lilinda</b> حَيَّ
- <b>lijengwa</b> بُنِيَ	- <b>lijenga</b> بَنَى

Tuagalie mifano kwenye sentensi:

المَبْنِي لِلْمَجْهُولِ (الماضي) Kauli ya kutendwa (uliopita)	المَبْنِي لِلْمَعْلُومِ (الماضي) Kauli ya kutenda (uliopita)
Nyumba ililindwa. الْمَنْزِلُ حُيِّ.	Mlinzi alilinda nyumba. الْحَارِسُ حَيَّ الْمَنْزِلَ.
Msikiti ulijengwa. الْمَسْجِدُ بُنِيَ.	Mjenzi alijenga msikiti. الْبِنَاءُ بَنَى الْمَسْجِدَ.

**NAMNA YA KUUNDA KAULI YA KUTENDWA KATIKA WAKATI ULIOPO**

- Katika vitenz vya wazi ( *Ajwaf* ) ( اجوف ) , herufi yake ya kwanza ipewe *Dhamma*, na herufi ya kabla ya mwisho lazima ibadilishwe na kuwa *alif* ( *l* ).

المَبْنِي لِلْمَجْهُولِ (المضارع) kauli ya kutendwa (uliop)	المَبْنِي لِلْمَعْلُومِ (المضارع) kauli ya kutenda (uliop)
-nafungwa يُصَامُ	-nafunga يُصُومُ
-nauzwa يُبَاعُ	-nauza يَبِيعُ

Tuagalie mifano kwenye sentensi:

المَبْنِي لِلْمَجْهُولِ (المضارع) kauli ya kutendwa (uliop)	المَبْنِي لِلْمَعْلُومِ (المضارع) kauli ya kutenda (uliop)
Mwezi wa ramadhani inafungwa. شَهْرُ رَمَضَانَ يُصَامَ.	Ali anafunga mwezi wa ramadhani.. عَلِي يُصُومُ شَهْرَ رَمَضَانَ.
Kitabu kinauzwa. الْكِتَابُ يُبَاعُ.	Mwenye duka anauza kitabu. التَّاجِرُ يَبِيعُ الْكِتَابَ.

- Katika vitenzi vya ( Naqis ) ( ناقص ) weka Dhamma kwenye herufi ya kwanza na weka fatha kwenye herufi ya mwisho na ubadilishe herufi ya mwisho ( ي او و ) kuwa alif .

kauli ya kutendwa (uliopo)	المَبْنِي لِلْمَجْهُول ( المضارع )	kauli ya kutenda (uliopo)	المَبْنِي لِلْمَعْلُوم ( المضارع )
- nalindwa	يُحَيِّ	- nalinda	يُحَيِّ
- najengwa	يُنَيِّ	- najenga	يُنَيِّ

Tuungalie mifano kwenye sentensi:

kauli ya kutendwa (uliopo)	المَبْنِي لِلْمَجْهُول ( المضارع )	kauli ya kutenda (uliopo)	المَبْنِي لِلْمَعْلُوم ( المضارع )
Nyumba inalindwa.	المَنْزِلُ يُحَيِّ.	Mlinzi analinda nyumba.	الْحَارِسُ يُحَيِّ الْمَنْزِلَ.
Msikiti unajengwa.	المَسْجِدُ يُنَيِّ.	Mjenzi anajenga msikiti.	الْبِنَاءُ يُنَيِّ الْمَسْجِدَ .

Hebu tuungalie muhtasari wa vitenzi visivyo vya kawaida ya kauli ya kutenda na kutendwa katika wakati uliopo na uliopita:

kauli ya kutenda (uliopo)	المَبْنِي لِلْمَعْلُوم ( المضارع )	kauli ya kutendwa (uliopo)	المَبْنِي لِلْمَجْهُول ( المضارع )	kauli ya kutenda (uliopita)	المَبْنِي لِلْمَعْلُوم ( الماضي )	kauli ya kutendwa (uliopita)	المَبْنِي لِلْمَجْهُول ( الماضي )
- nasema	يَقُولُ	- nasemwa	يُقَالُ	- lisema	قَالَ	- lisemwa	قِيلَ
- naahidi	يَعِدُ	- naahidiwa	يُوعَدُ	- liahidi	وَعَدَ	- liahidiwa	وُعِدَ
- nalia	يَبْكِي	- naliwa	يُبْكِي	- lililia	بَكَى	- lililiwa	بُكِيَ

## MATOKEO

Kutokana na uchunguzi wa njia na jinsi ya kuunda kauli ya kutendwa tunaweza kujumilisha kanuni za uundaji wa kauli ya kutendwa katika lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu kama ifuatayo:

- ❖ **Uundaji wa kauli ya kutendwa katika lugha ya Kiswahili** unagawanywa katika makundi matano na hufuata kanuni zifuatazo:

1. Vitenzi vinachukua kiambishi [ -WA ]  
Vitenzi vyenye asili ya Kibantu vinavyoishia na [Konsonanti + Irabu A] na [Irabu mbili IA]. Vitenzi vyenye asili ya Kiarabu vinavyoishia na [Irabu E] na [ Irabu I ]..
2. Vitenzi vinachukua kiambishi [ -LIWA ]  
Vitenzi vyenye asili ya Kibantu vinavyoishia na [ Irabu mbili AA ] na [ Irabu mbili UA ]. Vitenzi vyenye asili ya Kiarabu vinavyoishia na [ Irabu mbili AU ]
3. Vitenzi vinachukua kiambishi [ -LEWA ]  
Vitenzi vyenye asili ya Kibantu vinavyoishia na [Irabu mbili EA] na [ Irabu mbili OA ].
4. Vitenzi vinachukua kiambishi [ -IWA ]  
Vitenzi vyenye asili ya Kiarabu vinavyoishia na [ Irabu U ]
5. Vitenzi vya silabi moja  
Vitenzi vya silabi moja baadhi vyao vinachukua kiambishi [ - iwa ] na baadhi vyao vinachukua kiambishi [ -ewa ].

- ❖ **Uundaji wa kauli ya kutendwa katika lugha ya Kiarabu** inagawanywa katika makundi mawili na hufuata kanuni zifuatazo:

### 1- VITENZI VYA KIMSINGI VYA KAWAIDA

- Kauli ya kutendwa katika wakati uliopita huundwa kwa kuweka dhamma au fupi /o/ ( ُ ) kwenye herufi ya kwanza ya kitenzi, na kasrah au fupi /i/ ( ِ ) kwenye herufi kabla ya mwisho.
- Kauli ya kutendwa katika wakati uliopo huundwa kwa kuweka dhamma au fupi /o/ ( ُ ) kwenye herufi ya kwanza ya kitenzi, na fatha au fupi /a/ ( َ ) kwenye herufi kabla ya mwisho.

### 2- VITENZI VISIVYO VYA KAWAIDA:

#### • WAKATI ULIOPITA

- A. Katika vitenzi vya ( ajwaf ) ( اجوف ) herufi ya kwanza lazima ipewe Kasrah, na herufi ya kabla ya mwisho (yaani alif) lazima ibadilishwe kuwa yaa ( يي ).
- B. Katika vitenzi vya ( Naqis ) ( ناقص ) vinavyoishia na ( alif ) , weka Dhamma kwenye herufi ya kwanza na weka



*Kasrah* kwenye herufi ya kabla ya mwisho, kisha ubadilishe *alif* kuwa *yaa* ي.

Sharaf Aldin Alrajhi (1999)

شرف الدين الرجحي المبني للمجهول وتراكيبه ودلالته في القرآن الكريم - الإسكندرية 1999 م

#### • WAKATI ULIOPO

A. Katika vitenz vya wazi (*Ajwaf*) (اجوف), herufi yake ya kwanza ipewe *Dhamma*, na herufi ya kabla ya mwisho lazima ibadilishwe na kuwa *alif* (ل).

The Formation of Arabic Passive Verbs: Lexical or Syntactic?(n.d.).Retrieved from <http://Linguistics.huji.ac.il/IATL/25/laks.pdf>

B. Katika vitenzi vya *Naqis* (ناقص) weka *Dhamma* kwenye herufi ya kwanza na weka *fatha* kwenye herufi ya kabla ya mwisho na ubadilishe herufi ya mwisho (ي au و) kuwa *alif* ي.

TUKI. (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi, KE: OxfordUniversityPress.

Wahiga, G. (1999). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi, KE: Longhorn Publishers.

❖ Inaonekana wazi kwamba mojawapo wa sababu za shida la wanafunzi wa Kirabu kuelewa kauli ya kutendwa ni tofauti uliopo katika kanuni za uundaji wa kauli ya kutendwa kati lugha ya Kiswahili na Kiarabu.

#### MAPENDEKEZO

Kutokana na matekeo ya utafiti inaonekana wazi kwamba kuna haja kubwa ya kufanya utafiti unachunguza kauli ya kutendea, kauli ya kutendeka, kauli ya kutendana na kauli ya kutendesha.

#### MAREJEO

Ahmed Gish (2002)

أحمد قبش (2002) الكامل في النحو والصرف والإعراب، الجيل للطبع والنشر والتوزيع

Baraka, Y. (2018). *Unyambulishaji wa Vitenzi vya Lugha ya Kinyakusakatika Mkoa wa Mbeya-Kyela*. Morogoro, TZ: Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino.

Email Badie (2009)

إميل بديع يعقوب (2009) موسوعة النحو والصرف والإعراب دار العلم للملايين

E. Wesana chomi (2001) Misingi ya sarufi ya Kiswahili. Kituo cha utafiti wa mitaala ya Kiafrika.

Habwe na Karanja, (2004). Misingi ya Sarufi ya Kiswahili. Nairobi: Foenix Publishers.

Ibrahim Alsamrai (1986)

إبراهيم السامرائي الفعل زمانه وأبنيته، بيروت 1986 م

Khamis, A. M. (2008). *Maendeleo ya Uhusika, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Kihore, Y. M., D. P. B. Massamba na Y. P. Msanjila, , 2012 *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo*, Chapa ya 6, Dar es Salaam: TUKI.

Mbwillow, S. N. (2017). *Uambikaji kama Dhana Kuu: Tofauti ya Uambikaji na Unyambulishaji*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mohamed A. Mohamed (2006) *Sarufi Mpya*. Press and Publicity center.